BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Tano – Tarehe 12 Februari, 2019.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2018/2019.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

56. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Kwa kuwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeshaanza kufuatilia ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete juu ya matengenezo ya Barabara ya Fuoni Mtundani (meli sita) hadi skuli ya Kitongani.

Je, mchakato huo wa kufuatilia ahadi ya barabara hiyo umefikia wapi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

46. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Sheria ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mlaji ya mwaka 2018 inakataza mfanyabiashara kuwekewa vikwazo vya kusambaza au kununua bidhaa kwa lengo la kuleta ushindani katika uuzaji na utoaji wa huduma.

Je, kwa nini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imewazuia baadhi ya wafanyabiashara wa Konde kuuza vitunguu, viazi mbatata n.k ilhali wanawalipisha leseni za biashara.

115. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mnamo tarehe 31/12/2018 wakulima wa ndimu kutoka Wilaya ya Kusini Unguja wakiwa katika harakati ya kushusha ndimu zao katika soko la Mwanakwerekwe, Maafisa kutoka Halmashauri kwa mshangao walizuia ushushaji huo na kuwatoza faini wakulima hao kwa viwango tofauti baina kapu na polo.

(a) Je, ni kigezo gani walichokitumia kwa kikapu kuwatoza shs. 5,000/- na kipolo shs 8,000/-.

(b) Je, ni kiasi gani walichokusanya siku hiyo kwa adhabu hiyo.

(c) Je, Halmashauri haioni kitendo hicho kimewarudisha nyuma wananchi hao kutokana na ajira kuwa ngumu.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

76. MHESHIMIWA MASOUD ABRAHMAN MASOUD (Jimbo la Bububu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Tunaipongeza Serikali kwa kuwapatia fursa Mawakili wetu kufanya kazi kwa maslahi yao na ya Nchi yetu bila ya kubughudhiwa. Hata hivyo, baadhi ya Mawakili hususan wa kujitegemea hujiingiza katika usimamizi wa Mauziano ya Mali za wananchi na kuchukua asilimia ya mauziano hayo. Suala hili hupelekea kuikosesha mapato Serikali kwani baada ya mapato yale kwenda Serikalini yanaingia katika mifuko yao kwa maslahi yao.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.

(b) Kama inalifahamu, Je, Serikali imechukua hatua gani kulitatua hilo.

(c) Je, Serikali inatoa adhabu gani kwa wale wote wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

4. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Serikali inakiri kuwa kumuwezesha mwanamke ni kuiwezesha jamii.

(a) Je, mpaka sasa ni wanawake wangapi wamewezeshwa kwa kupatiwa mikopo ili kuwainua kiuchumi na kielimu.

(b) Je, ni kada zipi za wanawake ndizo zenye fursa zaidi za kuwapatia mikopo yenye lengo la kuwainua kiuchumi.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

41. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Mahitaji ya chakula hasa mchele ambao ndio chakula kikuu hapa Zanzibar ni tani 99,577 kwa mwaka, ambapo kiwango cha uzalishaji ni tani 25,794 tu sawa na 25.93%. Kwa kuwa ardhi tunayo na wataalamu wapo ambao watatuwezesha kupunguza tofauti ya uagiziaji wa mchele kutoka nje, jambo litakaloongeza ukuaji wa uchumi na pia kujitosheleza kwa chakula.

(a) Je, Serikali ina mpango gani ambao umejiwekea na utekelezaji wake ili kuitumia ardhi kuzalisha mpunga utakaotosheleza kwa chakula.

(b) Je, kuna utafiti gani uliofanywa ambao unaonesha uhalisia wa mavuno au kipato anachopata mkulima wa mpunga kwa kila eka moja.

(c) Je, Serikali ina mpango wa kujenga miundombinu ya kuhifadhia maji wakati wa mvua ili maji hayo yaweze kutumika wakati wa kiangazi.

Wizara ya Afya:

17. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali imefanya jitihada kubwa katika sekta ya afya ikiwemo kitengo cha uzazi salama kwa Serikali kulitafutia ufumbuzi suala la kupunguza vifo vya kina mama na watoto. Hata hivyo, suala hilo halijafanikiwa kwa asilimia mia pamoja na Wizara kufanya jitihada za kufanya maonesho kupitia wasanii lakini bado inaonekana lipo tatizo la amri sio hiari kwa familia hasa kwa upande wa mke au mume.

(a) Je, suala la uzazi salama kwa mama na mtoto ni tatizo kubwa au limepungua kwa asilimia ngapi kutoka 2015, 2016 mpaka 2017.

(b) Je, suala la elimu kwa kutumia wasanii na vikundi vya sanaa linatosha kumaliza tatizo hilo.

(c) Je, Wizara imefanya utafiti na kuona kwa nini tatizo la vifo vya mama na mtoto hutokea kwa wingi.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

58. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Miongoni mwa ahadi za Serikali katika kuimarisha miundombinu ya mawasiliano, ni kujenga barabara Fuoni hadi Tunguu kwa kiwango cha lami. Lakini ni muda mrefu sasa barabara hiyo imesita kutengenezwa.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kusita kutengenezwa.

(b) Ni lini kipande kilichobakia kutoka Fuoni Polisi hadi Tunguu kitakamilika.

III. HOJA ZA KAMATI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2018/2019.

Zanzibar,
12 Februari, 2019.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.